


BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI



TAARIFA KWA UMMA

UDAHILI KWA WAOMBAJI WA MAFUNZO YA ASTASHAHADA NA STASHAHADA KATIKA VYUO VYA MBALIMBALI KWA MWAKA WA MASOMO 2020/2021

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura ya 129, ili kusimamia na kuratibu utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo katika vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo. Jukumu mojawapo la Baraza ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo nchini yanakidhi vigezo na ubora unaohitajika katika soko la ajira ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Baraza linao wajibu wa kuratibu udahili wa wanafunzi kwenye Vyuo na kozi/programu zinazotambulika na mamlaka husika.

Dirisha la Udahili kwa mwaka wa masomo 2020/2021 lilifunguliwa tarehe 15 Juni, 2020 hadi tarehe 15 Septemba, 2020. Waombaji wa kozi za Astashahada na Stashahada walituma maombi ya kudahiliwa katika Vyuo mbalimbali. Baada ya dirisha la udahili kufungwa, Vyuo vilichagua waombaji wenye sifa kulingana na programu zinazotolewa. Waombaji waliochaguliwa waliwasilishwa NACTE kwa ajili ya UHAKIKI.

Jumla ya waombaji **79,045** walichaguliwa kujiunga na programu mbalimbali zinazotolewa na Vyuo **319** na kisha kuwasilishwa kwa ajili ya Uhakiki. Kati ya hao, jumla ya waombaji **73,308** (93%) wamekidhi vigezo vya kujiunga na programu walizochaguliwa, na waombaji **5,737** (7%) hawana vigezo vya kujiunga kwenye programu walizochaguliwa. Majibu ya Uhakiki huu yametumwa Vyuoni tayari.

Waombaji wote waliowasilishwa NACTE kwa ajili ya Uhakiki wametumiwa ujumbe na msimbo (*code*) kupitia simu na barua pepe walizowasilisha wakati wa kutuma maombi ya udahili. Msimbo huo unatumika kuhakiki kama wamechaguliwa au hawakuchaguliwa kupitia tovuti ya NACTE (www.nacte.go.tz). Kwa wale ambao hawakuchaguliwa kwa kutokuwa na sifa za kusoma programu walizoomba kama walivyowasilishwa na Vyuo walivyoomba, wanashauriwa kuomba upya kwenye Vyuo na programu wanazopenda.

Aidha, Baraza limefungua Dirisha la Awamu ya Pili la Udahili kuanzia leo **tarehe 15 hadi 26 Oktoba, 2020**. Wito unatolewa kwa wale waliokosa na wale ambao walikuwa hawajaomba kufanya hivyo kwakuwa hakutakwepo dirisha lingine la udahili kwa mwaka wa masomo 2020/2021.

Majina ya waombaji kwa Dirisha la Pili la Udahili wataochaguliwa na Vyuo yatawasilishwa NACTE kwa uhakiki kuanzia tarehe **27 hadi 30 Oktoba, 2020**. Matokeo ya uhakiki yatatolewa ifikapo tarehe **9 Novemba, 2020**. Masomo kwa waliochaguliwa yataanza rasmi kuanzia tarehe **15 Novemba, 2020**. Hivyo, wazazi na umma kwa ujumla waepuke kutapeliwa na wale wanaodai kwamba masomo yameanza kabla ya tarehe hiyo. Baraza pia linafuatilia kwa karibu kujua vyuo vyote ambavyo vinakiuka taratibu na hatua kali zitachukuliwa dhidi yao. Kama kuna wanafunzi ambao tayari wameitwa kuanza masomo au wataitwa kabla ya tarehe 15 Novemba, 2020 wawasiliane na Baraza kupitia barua pepe admissions@nacte.go.tz.

**IMETOLEWA NA:
OFISI YA KATIBU MTENDAJI
BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI (NACTE)
TAREHE: 15/10/2020**